

## **MAKALA**

### **DUWASA - MAMLAKA YA KWANZA YA MAJISAFI NA MAJITAKA KUPATA LESENI YA EWURA**

Mei 26, 2007 Dar es Salaam.

Naibu Waziri wa Maji Mh. Shamsa S. Mwangunga (Mbunge) ameipongeza Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Dodoma (DUWASA) kwa kuwa mamlaka ya kwanza ya maji kupata leseni ya EWURA. Pongezi hizo amezitoa katika sherehe ya utoaji wa leseni iliyofanyika katika hoteli ya Protea (Court Yard), iliyoko 'sea view' hapa jijini Dar Es Salaam. Alisema anapongeza DUWASA kwa kufikia hatua hiyo baada ya kufuzu mchakato wa kitaalam ulifanywa na EWURA. Pamoja na pongezi hizi, Naibu Waziri wa maji ameitaka DUWASA kuzingatia masharti yote yaliyowekwa kwenye leseni hiyo. Pia Naibu Waziri amezitaka Mamlaka zote za majisafi na majitaka ziwe zimepata leseni ifikapo mwishoni mwa mwezi Augosti 2007.

EWURA ni Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji. Sheria ya EWURA sura ya 414, inawapa EWURA mamlaka ya kutoa leseni kwa Mamlaka zote za majisafi na majitaka hapa nchini. Pamoja na Sekta ya Maji, EWURA pia inadhibiti utoaji wa huduma za sekta za nishati zikiwemo umeme, mafuta ya petroli na gesi asilia.

Akitoa maelezo ya utangulizi Mkurugenzi Mkuu wa EWURA Bw. Haruna Masebu alisema DUWASA inapaswa kufuata masharti ya leseni waliyopewa. Masharti hayo ni pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa huduma salama na endelevu ya majisafi na majitaka katika manispaa la Dodoma, DUWASA kuzingatia utunzaji wa mazingira wakati wote wanapotoa huduma na kutoa taarifa mara moja kwa EWURA pale itakapotokea kuwa DUWASA itashindwa kutoa huduma kwa mujibu wa masharti ya leseni.